

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF AGRICULTURE



TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES
AUTHORITY (TPHPA)



19th December, 203

TAARIFA KWA UMMA

SITISHO LA UAGIZAJI WA SOYA KUTOKA MALAWI

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) ni Shirika la Kitaifa la Hifadhi ya Mimea lililo anzishwa chini ya Wizara ya Kilimo kuitia Sheria No.4 ya 2020 ya Afya ya Mimea. TPHPA ina wajibu wa kudhibiti matumizi ya viuatilifu, kusimamia matakwa ya afya ya mimea, kudhibiti uingizaji na usafirishaji nje mimea na mazao ya kilimo na kuzuia uingiaji na usambaaji wa visumbufu vigeni.

Mamlaka inapenda kutoa taarifa muhimu kwa umma kuhusu uagizaji wa soya kutoka Malawi. Kuitia upembuzi unaondelea wa visumbufu hatarishi vyakarantini ili kuhuisha masharti ya kuingiza mazao nchini iliwemo soya kutoka Malawi, Mamlaka imebaini uwezekano mkubwa wa kuingia na kusambaa ugonjwa hatari wa virusi aina ya TRSV kwenye zao la soya ambao umeripotiwa kuwepo nchini Malawi..

Virusi vyakarantini ya TRSV ni hatarishi na huathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa zao la soya ambapo upotevu wa mazao shambani ni kati ya asilimia 25-100. Hatua ya kusitisha mara moja uagizaji wa soya na bidhaa zingine zitokanazo na soya ni muhimu katika kuzuia uingiaji na usambaaji wa kirusi hicho pamoja na kulinda uzalishaji wa zao hili hapa nchini.

Hatua hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Mimea ya mwaka 2020 na inahusu usitishaji wa uagizaji wa soya kutoka malawi pamoja na ile inayosafirishwa kwenda nchi zingine kuitia mipaka ya nchi yetu mpaka pale itakapoamuliwa viginevyo.

Mamlaka inatoa wito kwa waagizaji, wadau na wafanyabiashara wote wa soya nchini kuzingatia zuio hili. Mamlaka inashauri waagizaji kuendelea kuagiza soya kutoka nchi zingine ambazo hazina tishiao hili la ugonjwa wa virusi vyakarantini ya TRSV.

Tunashukuru kwa ushirikiano wenu.

Prof. Joseph C. Ndunguru
MKURUGENZI MKUU